**Faragha yako ni muhimu kwetu.** Sera hii ya faragha imeundwa na kusasishwa ili kuwahudumia vyema wale walio na haja ya kujua jinsi 'Taarifa yao Binafsi ya Utambulisho (Personally Identifiable Information, PII)' inavyotumika mtandaoni. PII, kama inavyofafanuliwa katika sheria ya faragha ya Marekani na usalama wa taarifa, ni taarifa inayoweza kutumika yenyewe au pamoja na taarifa nyingine kutambua, kuwasiliana au kumtafuta mtu. Tafadhali soma sera yetu ya faragha kwa makini ili upate ufahamu wazi wa jinsi tunavyokusanya, kutumia, kulinda au kushughulikia kwa njia nyingine Taarifa ya Binafsi ya Utambulisho kwa mujibu wa tovuti yetu na programu ya na *Count the Kicks*

Je, ni taarifa gani ya kibinafsi tunayochukua kutoka kwa watu wanaotembelea tovuti yetu naprogramu ya *Count the Kicks* ?

Unapounda wasifu kwenye programu yetu, inavyofaa, unaweza kuombwa uweke jina lako, anwani ya baruapepe, msimbo wa posta, nambari ya simu au taarifa nyingine ili kukusaidia kwa matumizi yako.

Unapotoa mchango au kuagiza vifaa kwenye tovuti yetu, inavyofaa, unaweza kuombwa uweke jina lako, anwani ya baruapepe, anwani ya barua, nambari ya simu au taarifa nyingine ili kukusaidia kwa matumizi yako au kukutumia nyenzo za kielimu.

Je, ni wakati gani tunachukua taarifa?

tunachukua taarifa kutoka kwako unapounda wasifu au unapoingiza taarifa kwenye tovuti au programu yetu, au kujiandikisha katika ujumbe wa SMS.

Je, tunatumiaje taarifa yako?

Tunaweza kutumia taarifa tunayochukua kutoka kwako unapounda wasifu, unapojiandikisha kwa ajili ya kupata jarida letu, unapojiandikisha katika ujumbe wa SMS, unapojibu utafiti au mawasiliano ya uuzaji, au kutumia vipengele vingine vya tovuti katika njia zifuatazo:

- Kuturuhusu kukuhudumia vyema zaidi katika kujibu maombi yako ya huduma kwa wateja
- Kubinafsisha hali yako ya matumizi na kuturuhusu kuwasilisha aina ya maudhui ambayo unapendelea zaidi
- Kutoa matangazo, utafiti au kipengele kingine cha tovuti
- Kuomba ukadiriaji na taathmini ya huduma au bidhaa
- Kukufuatilia baada ya mawasiliano (baruapepe, ujumbe mfupi, au maswali kwa njia ya simu)

Je, tunalinda taarifa yako vipi?

Tovuti yetu inachanganuliwa mara kwa mara ili kuchunguza ukosefu wa usalama na udhaifu unaojulikana ili kufanya ziara yako kwenye tovuti yetu iwe salama iwezekanavyo. Tunatumia Uchanganuzi wa Programu Hasidi mara kwa mara.

Taarifa yako ya kibinafsi inahifadhiwa kwenye mitandao iliyolindwa na inaweza kufikiwa na idadi ndogo tu ya watu walio na haki maalum za kufikia mifumo kama hiyo, na wanatakiwa kuweka taarifa hayo kuwa

ya siri. Tunatekeleza hatua mbalimbali za usalama mtumiaji anapoingiza, kuwasilisha, au kufikia taarifa yake ili kudumisha usalama wa taarifa yako ya kibinafsi.

Shughuli zote huchakatwa kupitia mtoa huduma wa njia kuu na hazihifadhiwi au kuchakatwa kwenye seva zetu.

Kufichuliwa kwa wahusika wengine

**Hatuuzi** , hatufanyi biashara au kuhamisha kwa watu wa nje Taarifa yako Binafsi ya Utambulisho.

Viungopepe vya wahusika wengine

Mara kwa mara, kwa uamuzi wetu, tunaweza kujumuisha au kutoa bidhaa au huduma za wahusika wengine kwenye programu yetu. Tovuti hizi za wahusika wengine huwa na sera tofauti za faragha na huru. Kwa hivyo hatuna wajibu au dhima kwa maudhui na shughuli za tovuti hizi zilizounganishwa. Hata hivyo, tunataka kulinda uadilifu wa tovuti yetu na tunakubali maoni yoyote kuhusu tovuti hizi.

Kanuni ya Ulaya ya Ulinzi wa Data (General Data Protection Regulation, GDPR)

GDPR ilianza kutumika tarehe 25 Mei, 2018 na inadhibiti jinsi tunavyowasiliana na watumiaji katika Muungano wa Ulaya. Tumechukua hatua zifuatazo ili kuhakikisha kwamba tunafuata GDPR:

- Kusasisha sera hii ya faragha ili tufuate GDPR.
- Kutuma mawasiliano ya baruapepe ili kuwafahamisha kuhusu masasisho hiya.
- Tunaripoti ukiukaji wowote wa sera ya faragha ya data ya Ulaya kwa mdhibiti wa Muungano wa Ulaya ndani ya saa 72.
- Kufuata matakwa ili kulinda mifumo na data kwa mipango bora ya kiusalama.
- Tuna uwezo wa kukubali maombi yanayotumia haki za mtu binafsi za kufikia, kusahihisha, kufuta na kuhamisha taarifa ya kibinafsi. Unaweza kuomba data yako ifutwe kabisa wakati wowote. Iwapo ungependa kuomba data yako ifutwe, tafadhali tutumie baruapepe info@countthekicks.org.
- Tuna uwezo wa kukubali ombi la mtu binafsi la kuzuia au kupinga kuchakatwa kwa data ya kibinafsi na kupinga uamuzi wowote kulingana na kuchakatwa kwa data ya kibinafsi kiotomatiki.

Sheria ya California ya Ulinzi wa Faragha ya Mtandaoni

CalOPPA ni sheria ya kwanza ya serikali katika taifa inayohitaji tovuti za kibiashara na huduma za mtandaoni kuchapisha sera ya faragha. Kwa mujibu wa CalOPPA, tunakubaliana na yafuatayo:

- Watumiaji wanaweza kutembelea programu yetu bila kujitambulisha.
- Unaweza kupata sera hii ya faragha kwenye tovuti yetu, www.countthekicks.org. Utajulishwa kuhusu mabadiliko yoyote ya Sera ya Faragha kwenye Ukurasa wetu wa Sera ya Faragha.

- Watumiaji wanaweza kubadilisha taarifa ya kibinafsi kwa kuingia kwenye akaunti zao.

Je, tovuti yetu inashughulikia vipi ishara za Usifuatilie?

Tunaheshimu ishara za Usifuatilie na Hatufuatulii, kuweka vidakuzi, au kutumia matangazo wakati kipengele cha kivinjari cha Usifuatilie (Do Not Track, DNT) kimewashwa.

Haturuhusu ufuatiliaji wa mienendo ya watu wengine.

Sheria ya Ulinzi wa Faragha ya Watoto Mtandaoni (Children Online Privacy Protection Act, COPPA)

Inapohusu suala la ukusanyaji wa taarifa ya kibinafsi kutoka kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka 13, Sheria ya Kulinda Faragha ya Watoto Mtandaoni (COPPA) inawapa wazazi kuwa na udhibiti. Tume ya Shirikisho la Biashara, shirika la ulinzi wa watumiaji wa Marekani, hutekeleza Kanuni ya COPPA, ambayo inaeleza kile ambacho waendeshaji wa tovuti na huduma za mtandaoni wanapaswa kufanya ili kulinda faragha na usalama wa watoto mtandaoni.

Hatuuzi haswa kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka 13.

Mienendo Bora Kuhusu Taarifa

Kanuni za Mienendo Bora Kuhusu Taarifa zinaunda uti wa mgongo wa sheria ya faragha nchini Marekani na dhana zinazojumuisha zimekuwa na jukumu kubwa katika uundaji wa sheria za kulinda data duniani kote. Kuelewa Kanuni za Mienendo Bora Kuhusu Taarifa na jinsi zinafaa kutekelezwa ni muhimu ili kuzingatia sheria mbalimbali za faragha zinazolinda taarifa ya kibinafsi.

Ili kufuata Mienendo Bora Kuhusu Taarifa, tutakuarifu kupitia baruapepe ndani ya siku 1 ya kazi ikiwa kumekuwa na ukiukaji wa data.

Pia tunakubaliana na Kanuni ya Usuluhishi wa Mtu Binafsi ambayo inahitaji kwamba watu binafsi wawe na haki ya kufuatilia kisheria haki zinazoweza kutekelezeka dhidi ya wanaochukua na wanaochakata data ambao wanashindwa kuzingatia sheria. Kanuni hii haihitaji tu kwamba watu binafsi wawe na haki zinazoweza kutekelezeka dhidi ya watumiaji wa data, lakini pia kwamba watu binafsi wanaweza kwenda mahakamani au katika mashirika ya serikali kuchunguza na/au kushtaki kuwa wachakataji wa data hawafuati kanuni.

Sheria ya CAN SPAM

Sheria ya CAN-SPAM ni sheria inayoweka masharti kuhusu baruapepe za kibiashara, kuimarisha matakwa ya ujumbe wa kibiashara, kuwapa wapokeaji haki ya kukomesha baruapepe kutumwa kwao, na inaelezea adhabu kali za ukiukaji.

tunachukua anwani yako ya baruapepe ili:

- Kutuma taarifa, kujibu maswali na/au maombi au maswali mengine
- Kupata soko kwa orodha yetu ya wanaopokea baruapepe au kuendelea kutuma baruapepe kwa wateja wetu baada ya muamala wa kwanza kutokea.

Ili kufuta CANSPAM, tunakubaliana na yafuatayo:

- Kutotumia mada au anwani za baruapepe zisizo za kweli au za kupotosha.
- Kutambua ujumbe kama tangazo kwa njia inayofaa.
- Kujumuisha anwani halisi ya makao makuu ya biashara au tovuti yetu.
- Kufuatilia utiifu wa huduma za uuzaji kupitia baruapepe kwa wahusika wengine, ikiwa moja inatumika.
- Kuheshimu maombi ya kujiondoa haraka.
- Kuruhusu watumiaji kujiondoa kwa kutumia kiungopepe kilicho sehemu ya chini ya kila baruapepe.

Ikiwa ungependa kujiondoa kwa kupokea baruapepe za siku zijazo au iwapo una maswali kuhusu sera hii ya faragha, unaweza kututumia baruapepe katika info@countthekicks.org